

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA MJI GEITA

MKOA WA GEITA

Simu No. 0282520437
Nukuhi No. 0282520437
Barua Pepe: td@geitac.go.tz
Tovuti : www.geitac.go.tz



**Halmashauri ya Mji,
S.L.P 384,
GEITA.**

TAREHE: 26/05/2020

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA DEREVA WA MITAMBO DARAJA II – NAFASI 3

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita anawatangazia nafasi za kazi na anakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa za kujaza nafasi za uendeshaji wa mitambo ya “**Roller, Excavator na Grader**” kama ilivyoorodheshwa katika tangazo hili;-

1.0 MAJUKUMU YA KAZI

- Kuendesha mitambo chini ya usimamizi wa dereva mitambo mwenye uzoefu.
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa.

2.0 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
- Kuajiriwa mwenye leseni ya daraja G ya uendeshaji Mitambo.

NB: Wenye leseni zenye sifa za ziada kama daraja F, E na C1 watapewa kipaumbele.

3.0 MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (Detailed CV) yenye anuani ya Posta na namba ya simu ya kuaminika ikiambatana na majina ya wadhamini watatu (3).
- Maombi yaambatanishwe na nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo ya uendeshaji wa mitambo na vyeti vya kidato cha Nne vilivyodhibitishwa na Mwanasheria.
- Muombaji aambatanishe picha ndogo ya rangi (passport size) ya hivi karibuni.
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form VI and form IV result slips) HAVITAKUBALIWA.
- Waombaji waliosoma elimu ya kidato cha nne (4) nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA).
- Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma wapitishwe barua zao za maombi ya kazi kwa waajiri wao.
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

4.0 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya mshahara TGOS A kwa mwezi.

5.0 UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **15/06/2020** saa **9:30** alasiri. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwenda kwa Mkurugenzi, Halmashauri ya Mji, **S.L.P 384 GEITA**. Waombaji watakaokidhi vigezo watajulishwa kwa njia ya simu na matangazo ili kuweza kuja kwenye usaili.

Eng. Modest J. Apolinary,
**MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MJI,
GEITA.**